# JARIDA LA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

*Wizara ya Furaha*

Toleo Maalum la: 21 | 30 Juni, 2021 | www.habari.go.tz

# FAINALI ZA KIHISTORIA MASHINDANO YA UMISSETA 2021



# YALIYOJIRI KATIKA WA MASHINDANO YA MICHEZO YA UMISSETA

## 30 Juni, 2021

**KAULIMBIU: "MICHEZO SANAA NA TAALUMA KWA MAENDELEO YA UCHUMI WA VIWANDA"**

# NUKUU YA KATIBU MKUU WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO DKT. HASSAN ABBASI

Sasa tunaangalia uwezekano wa kuwa na kanda za UMISSETA na UMISHUMTA kwa maana ya kuwa na kanda au mikoa itakayochaguliwa maalum na shule maalum zenye miundombinu ya michezo ili miundombinu ya kisasa iongezewe kwenye shule hizo.

Hii itawafanya vijana wetu sasa waweze kucheza katika mazingira ya kiwango cha kimataifa ili wakienda kwenye mashindano ya kimataifa waone mazingira yanafanana na hapa nyumbani hatimaye waendelee kufanya vizuri zaidi.

**DKT. HASSAN ABBASI**

**Katibu Mkuu – Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.**



**KATIBU MKUU WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO DKT. HASSAN ABBASI AKIWA AMEAMBATANA NA MKUU WA WILAYA YA MTWARA DUNSTAN KYOBYA NA MKURUGENZI WA MAENDELEO YA MICHEZO YUSUPH SINGO LEO WAKATI AKIKAGUA MCHEZO WA NUSU FAINALI BAINA YA MTWARA (WENYE BLUU) NA DODOMA (WENYE NYEKUNDU).**





# ARUSHA MABINGWA MCHEZO WA KURUSHA MKUKI UMISSETA 2021

Mikoa ya Arusha na Dodoma imeongoza kwenye mchezo wa kurusha Mkuki katika Mashindano ya Taaluma na Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) kwenye fainali zilizofanyika leo Juni 30, 2021 uwanja A kwenye chuo cha walimu mjini Mtwara.

Msemaji wa UMISSETA 2021, John Mapepele amesema Elisha Leiya kutoka Arusha ameibuka kuwa mshindi wa kwanza baada ya kurusha umbali wa mita 51 na sentimita 20 akifuatiwa na Yohana Nichorausi kutoka mkoa wa Mwanza aliyerusha umbali wa mita 47 na sentimita 26 wakati nafasi ya atu imechukuliwa na Rajabu Mtonyi kutoka Mkoa wa Dodoma aliyerusha umbali wa mita 45 na sentimita 70.

Kwa upande wa wasichana Joyce Barnaba kutoka Mkoa wa Dodoma ndiye Mshindi wa kwanza kwa kurusha mita 32 na sentimita 25 akifuatiwa na Fatma Saidi kutoka Unguja aliyerusha umbali wa mita 31 na sentimita 35 ambapo nafasi ya tatu ilichukuliwa na maria Gamalile kutoka Manyara liyerusha umbali wa mita 30 na sentimita 42.

# TIMU ZINAZOINGIA FAINALI MICHEZO YOTE UMISSETA 2021

Michezo inayoendelea kwenye Mashindano ya Taaluma na Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) yanafikia fainali kesho Julai 1, 2021 kwenye viwanja mbalimbali vya mjini Mtwara ambapo mashindano hayo yatafungwa rasmi Julai 2,2021.

Kwa mujibu wa Msemaji wa mashindano hayo, John Mapepele fainali ya soka kwa wavulana itakuwa baina ya timu ya Pemba na Mtwara na itachezwa siku ya kufunga mashindano hayo Julai 2,2021 katika uwanja wa Nangwanda Sijaona wakati mchezo wa kumtafuta mshindi wa tatu soka utachezwa kesho baina ya timu ya mkoa wa Dodoma na Geita.

Amesema mchezo wa Soka kwa upande wa wasichana utakuwa baina ya timu ya mkoa wa Mwanza na Tabora ambao utachezwa kesho mchana Julai 1,2021 ambapo hadi sasa mshindi wa tatu ni mkoa wa Arusha.

Pia fainali ya Mpira wa Pete itakuwa dhidi ya timu ya mkoa wa Mwanza na Songwe.

Kwa upande wa mpira wa Wavu fainali wasichana itachezwa baina ya mkoa wa Dar es Salaam na Mtwara wakati wavulana itakuwa kati ya Dar es Salaam na Arusha.

Mpira wa mikono fainali wasichana itakuwa baina ya mkoa wa Songwe na Morogoro na kwa upande wa wavulana Unguja watakipiga na Tabora.

Kwa upande wa mpira wa kikapu fainali kwa wanaume itakuwa baina ya Unguja na Dar es Salaam wakati kwa upande wa wanawake itakuwa baina ya Dar es Salaam na Mwanza.

# MCHEZAJI WA SIKU




Kila mchezo unahitaji kuupenda na kuufanyia mazoezi ya kutosha. Nimekuwa nikifanya mazoezi ya kutosha kila wakati nikiwa likizo.

Nimefurahi kuwa mshindi wa kwanza kwenye mashindano ya mwaka huu, nimeweza kutupa umbali wa mita 51 na sentimita 20.

Naishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuendelea kuuweka mchezo huu kwenye michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA.

**ELISHA LEIYA**

**Mshindi wa kwanza wa kurusha Mkuki**
**UMISSETA 2021 – Mkoa wa Arusha**

# MPIRA WA MIKONO WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA MIKONO KWA WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 30, 2021. TIMU ZA MIKOA YA DAR ES SALAAM 16 (WENYE NJANO) NA TABORA 21 (WENYE NYEUSI).





# MPIRA WA MIKONO WASICHANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA MIKONO KWA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 30, 2021. TIMU ZA MIKOA YA GEITA 19 (WENYE BLUU BAHARI) NA SONGWE 28 (WENYE MACHUNGWA).





# MPIRA WA KIKAPU WASICHANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA KIKAPU KWA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 30, 2021. TIMU ZA MIKOA YA DAR ES SALAAM 72 (WENYE KIJANI) NA KILIMANJARO 36 (WENYE BLUU BAHARI)





# MPIRA WA KIKAPU WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA KIKAPU KWA WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 30, 2021. TIMU ZA UNGUJA 59 (WENYE BLUU) NA PEMBA 31 (WENYE NJANO).





# MPIRA WA KIKAPU WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA KIKAPU KWA WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 30, 2021. TIMU ZA UNGUJA 63 (WENYE KIJANI KIBICHI) NA MWANZA 57 (WENYE NYEKUNDU).





# MPIRA WA WAVU WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA WAVU KWA WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 30, 2021. TIMU ZA UNGUJA 2 (WENYE NJANO) NA DAR ES SALAAM 3 (WENYE BLUU).





# MPIRA WA WAVU WASICHANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA WAVU KWA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 30, 2021. TIMU ZA MIKOA YA DAR ES SALAAM 3 (WENYE BLUU) NA MARA 0 (WENYE BLUU MISTARI MYEUPE).





# MPIRA WA MIGUU WASICHANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA MIGUU KWA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 30, 2021. TIMU ZA MIKOA YA ARUSHA 3 (WENYE BLUU) NA LINDI 0 (WENYE NYEUSI).





# MPIRA WA MIGUU WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA MIGUU KWA WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 30, 2021. TIMU ZA MIKOA YA MTWARA 1 (WENYE NYEUPE) NA DODOMA 0 (WENYE NYEKUNDU).






# MPIRA WA MIGUU WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA MIGUU KWA WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 30, 2021. TIMU ZA PEMBA 4 (WENYE KIJANI) NA GEITA 3 (WENYE BLUU BAHARI).





# MASHINDANO YA RIADHA
## MBIO ZA KUPOKEZANA VIJITI – WAVULANA

**KUNDI LA WASHIRIKI KUTOKA PEMBA LIMEIBUKA KUWA WASHINDI WA KWANZA KWA MBIO ZA KUPOKEZANA VIJITI MITA 4 X 100 (RELAY).**






# MASHINDANO YA RIADHA
# MBIO ZA KUPOKEZANA VIJITI – WASICHANA

## KUNDI LA WASHIRIKI KUTOKA TABORA LIMEIBUKA KUWA WASHINDI WA KWANZA KWA MBIO ZA KUPOKEZANA VIJITI MITA 4 X 100 (RELAY)






# MASHINDANO YA RIADHA
## KURUSHA MKUKI – WAVULANA

**ELISHA LEIYA KUTOKA ARUSHA AMEIBUKA KUWA MSHINDI WA KWANZA BAADA YA KURUSHA UMBALI WA MITA 51 NA SENTIMITA 20.**



# MASHINDANO YA RIADHA
## KURUSHA MKUKI – WASICHANA

**JOYCE BARNABA KUTOKA MKOA WA DODOMA NDIYE MSHINDI WA KWANZA KWA KURUSHA MITA 32 NA SENTIMITA 25.**



UMITASHUMTA | UMISSETA 2021

# #MwakaWaVipaji

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
S.L.P 25, 40470 DODOMA, TANZANIA

www.habari.go.tz